Defending Human Rights Defenders

The Human Rights Centre Uganda

# MAELEKEZO YA KUWAKILISHA MADAI SHUTUMA ZA UKIUKAJI WA AZIMIO LA UMOJA WAMATAIFA KUHUSU WALINZI WA HAKI ZA BINADAMU KWA KATIBU MAALUM WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU HALI YA WALINZI WA HAKI ZA BINADAMU



Defending Human Rights Defenders

The Human Rights Centre Uganda

# MAELEKEZO YA KUWAKILISHA MADAI SHUTUMA ZA UKIUKAJI WA AZIMIO LA UMOJA WAMATAIFA KUHUSU WALINZI WA HAKI ZA BINADAMU KWA KATIBU MAALUM WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU HALI YA WALINZI WA HAKI ZA BINADAMU



## UTANGULIZI:

Azimio la Umoja wa mataifa kuhusu watetezi wa Haki za kibinadamu linaeleza kuwa, kila binadamu/mtu ana wajibu wa kuunga mkono na kulinda haki za kibinadamu kwa uwiano. Kijitabu hiki, kimeandaliwa na Kituo cha Shirika la haki za Kibinadamu cha Uganda, kwa lengo la kuwaunga mkono watetezi wa haki za kibinadamu, kwa kazi yao ya busara sana. Imebainika kuwa, watetezi wengi wa haki za kibinadamu wanaoendesha kazi mbalimbali za haki za kibinadamu, wanapata shida, na wakati mwingine, hawajui taratibu za kiulinzi zilizoko kwa manufaa yao. Tunataka kuwapa furusa watetezi wote wa haki za kibinadamu, kushiriki moja kwa moja kwa taratibu zote. Na kijitabu hiki kimelengwa kuwa kama chombo cha kutumiwa kivitendo, kwa watetezi wote wa haki za kibinadamu, wanaotaka kusambaza taarifa inayohusiana na madai ya uvunjaji wa hako za kibinadamu, kwa taratibu zozote maalumu. Kijitabu hiki kimefasiriwa/kimetafsiriwa kwa lugha saba za kienyeji zinazozungumzwa mno nchini Uganda. Lugha hizo ni: Acholi, Ateso, Kiswahili, Lango, Luganda, Runyankore, Rukiga, Runyoro na Rutooro.

Pongezi maalumu zifikie Ubalozi wa Ufalme wa Norway, na shirika la "Irish Aid" kwa misaada ya kifedha, iliyotolewa kuelekea mradi huu.

© 2011

## KUCHAGUA NA KUPATA HABARI ZA KWELI.

- Kabla ya kuwakilisha lalamiko lolote, hakikisha kwamba habari zote kamili zimepatikana.
- Ukiwa na habari ya ziada ambayo ni muhimu ni bora. Ifuatayo ni mifano ya kutoa habari ya ziada. Habari ya ziada si wajibu lakini inaweza ikawa muhimu kwenye baadhi ya kesi mbali mbali.

## KUTUNZA SIRI

Maelezo ya mtu aliyeathirika yatakuwa kwenye mawasiliano ya Umoja wa Mataifa na Taifa linalohusika kwa kupitia katibu maalum wa Umoja wa Mataifa. Umoja wa Mataifa hauwezi kuingilia kati bila ya kueleza jina na maelezo ya muathiriwa. Ikiwa mhusika yuko chini ya umri wa miaka 18, muandishi/katibu maalum wa Umoja wa Mataifa ataweka jina la muathiriwa huyo kwenye mawasiliano na Taifa husika, lakini katibu/muandishi maalum hayataweka jina la muathiriwa kwenye ripoti ya wazi. Muathiriwa anaweza akaomba jina lake lisiwekwe kwenye ripoti ya wazi.

Chanzo cha habari ya shutuma za ukiukwaji ni siri, isipokuwa chanzo hicho cha habari kikikubali kutajwa. Habari ikiwa inatolewa, lazima mtu aeleze habari itakayofichwa ndani yake.

## HABARI MUHIMU

### 1. Jina la muathiriwa au waathiriwa.

Ni muhimu kutaja jina la kwanza na majina ya familia na majina hayo yaandikwe kikamilifu. Kwa mfano jina : Yiga Matovu.

**(Waathiriwa wanaweza kuwa watu binafsi, mashirika au makundi mbali mbali. )**

### 2. Hali ya muathiriwa kama mlinzi wa haki za binadamu.

Pindi ambapo mlinzi wa haki za Binadamu (watu au mashirika ) ni mtuhumiwa? Kwa mfano mwanawake mlinzi wa haki za Binadamu, muandishi wa habari, haki za watoto na kadhalika.

- Ikiwa muathiriwa ni mtu binafsi, tafadhali toa habari kuhusu jinsia, umri, uraia na shughuli anayoifanya.
- Ikiwa muathiriwa ni mtu binafsi au ni shirika, tafadhali eleza anwani ya mhusika.

Anwani ya mhusika inachukuliwa kama siri.

- Ikiwa ni muhimu na lazima, tafadhali onyesha Taifa, mji mkuu wa mtu, watu au mashirika yanayohusika na kazi hii ya ulinzi wa haki za binadamu.

**3. Ukiukwaji uliofanyiwa dhidi ya muathiriwa.**

Nini kilichofanyika? Wapi? Lini? Hali iliopo wakati huo.

**4. Wakiukaji.**

Toa habari yoyote ya watu walioshukiwa kutenda ukiukaji, kwa mfano wanaume wawili ( kwenye mavazi rasmi); cheo, sehemu ya kazi, walivyovaa au wanavyofanana na cheo cha heshima.

**5. Mashahidi.**

Kulikuwepo mashahidi wowote wakati wa ukiukwaji? Kulikuwepo walioathirika wowote?

**6. Hatua zilizochukuliwa na uongozi uliopo wakati huo.**

Kitendo hicho kilisemwa kwenye uongozi uliopo wakati huo.

Hatua gani iliochukuliwa ?

**7. Hatua iliochukuliwa na muathiriwa au na mashirika ya haki za Binadamu.**

Ukiukwaji huo umewekwa hadharani?

Habari hii ya ukiukwaji huu wa haki za Binadamu imetumwa kwenye mashirika mengine ya haki za Binadamu?

**8. Mahusiano kati ya ukiukwaji wa haki za Binadamu na kazi ya haki za Binadamu.**

Kwa nini unahisi ukiukwaji unahusiana na kazi ya ulinzi wa haki za Binadamu wa muathirika?

Wakati kitendo cha ukiukwaji wa haki za Binadamu kinaposababisha vitendo vingine, tafadhali elezea vitendo hivyo kwa mpangilio na jinsi vilivyoanza. Kwa mfano, ikiwa sababu kuu ilikuwa mlinzi wa haki za Binadamu amekamatwa, maelezo zaidi yatolewe. Ikiwa mtu huyo anafungwa mara kwa mara, habari zaidi

inaweza kuhusu; sehemu alipofungiwa, ikiwa mtu huyo aliyefungwa anaweza kupata hakimu, masharti ya kifungo, hatia na kadhalika.

## 9. Matokeo ya wali au matekeo ya zamani.

Ikiwa kuna matokeo ya awali ambayo ni muhimu yanayohusiana na tokeo hili, tafadhali toa maelezo zaidi.

## 10. Nani anayetoa habari hii?

(Siri)

Eleza jina na anwani. Eleza kazi anayofanya, ikiwa ni muhimu.

Maelezo yanaweza yakatolewa na mashirika au na mtu binafsi.

## 11. Habari mpya za mara kwa mara.

Tafadhali, tuma habari upya ya mara kwa mara haraka iwezekanavyo. Ni muhimu kufahamu ikiwa kuna mabadiliko ya hali ya afya ya muathirika

Habari mpya ya mara kwa mara inaweza kutolewa kama;

- Habari ya ziada itakapojulikana ( kwa mfano maelezo ya mtu aliyefanya ukiukwaji)
- Matokeo mapya yanayojitokeza ( kwa mfano muathiriwa anapotoka kwenye kifungo)

## Mfano wa barua kwa katibu/muandishi maalum wa walinzi wa haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa.

Bi. Stella Wanyana, Hakimu, anayeishi (jina la nchi na mji kuu). Stella Wanyana anawakilisha na kuendeleza kesi ya watu wa hali ya chini ili wapate haki ya nyumba nzuri za kuiishi.

Pia ni mwanachama wa mahakimu wanawake nchini Uganda.

Stella Wanyana alipata vitisho kuhusu usalama wake. Kulingana na habari tulizonazo, ( siku/mwezi/mwaka) Bi. Stella Wanyana alipokea barua ofisini kwake (jina la mji/mji mkuu). Barua ilikuwa na anwani yake, mlikuwemo maneno “ Chunga sana” au “Kuwa mwangalifu”. Baadaye siku hiyo Bi Stella Wanyana alipokuwa anaendesha gari kutoka ofisini kwenda nyumbani alifuatiliwa kwa karibu sana na wanaume wawili waliokuwa kwenye gari jeupe.

Stella Wanyana hakuweza kuwatambua wanaume waliokuwa wakimfuatilia wala hakutambua gari lao. Rafiki aliyekuwa na Stella Wanyana kwenye gari aliona pia gari likiwafuatilia. Stella Wanyana alipeleka mashtaka ya matokeo yote mawili kwenye kituo cha Polisi (jina/anwani ya kituo) siku hiyo. Polisi ilianzisha upelelezi. Pia alipeleka habari ya matokeo hayo mawili kwenye gazeti la kawaida ( jina).

Baada ya mwaka mmoja (tarehe) Hakimu mwengine aliyekuwa anawakilisha kikundi alichokuwa anawakilisha Bi. Stella Wanyana alipata barua ya vitisho kama ile alioipata Bi. Stella Wanyana, na baadaye ( tarehe) mtu huyo aliuliwa/aliuawa na watu wasiojulikana.

Barua hii imetumwa na chama cha wanawake mahakimu wa Uganda, mahali anapofanya kazi Stella Wanyana.

## Habari ya ziada

(Miezi miwili baadaye) tumefahamu leo (tarehe) kwamba upelelezi wa Polisi ulisimamishwa jana. Wanaume wawili walikamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi kwa kosa la kutuma barua ya vitisho kwa Stella Wanyana ( tarehe) na kumufuatilia na gari alipokuwa anatoka kazini kwenda nyumbani siku iliyofuata. Wanaume hao watapelekwa mahakamani kwenye muda wa wiiki mbili.

Bi. Stella alifurahishwa na kukamatwa kwa watu hao lakini anaamini kwamba mtu aliyeamrisha vitendo hivyo bado yuko huru. Aliomba Polisi iendelee na upelelezi.

## Anwani ya kutuma maelezo na habari zaidi kwa Umoja wa Mataifa.

- Wafanya kazi wa Umoja wa Mataifa watahakikisha kupata kwa maelezo yaliotumwa ikiwa kuna maombi ya kufanya hivyo. Wafanyakazi wanapatikana wakati wowote kwa majadiliano zaidi.
- Barua pepe, (E-mail) ni; urgent-action@ohchr.org Kichwa cha habari kiwe “walinzi wa haki za Binadamu”
- Fax, +41229179006. (Geneva Switzerland)
- Simu, +4122917123. Hii ni nambari ya mpokeaji wa simu wa Umoja wa Mataifa mjini Geneva, Switzerland. Watu waombe kuongea na wafanyakazi wa Tume ya haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa; tume inayohusuika na haki za Binadamu, haswa wafanyakazi wanohusika na kutoa kazi ya msaada kwa mwandishi maalum wa tume ya walinzi wa haki za Binadamu.

**The Human Rights Centre Uganda**,
P. O. Box 25638, Kampala,
Uganda.

Telephone: +256 414 266186
E-mail: hrcug@hrcug.org
Website: www.hrcug.org